

ISHI UWEZO WAKO

Jinsi Ya Kutumia Uwezo Wako Wa Kipekee Kwa 100%

KUHUSU KITABU

Tunaishi katika dunia ambayo watu wengi wanajua mambo mengi sana lakini wanafanya kidogo na wengine hawafanyi kabisa.

Ni katika dunia ambayo watu wengi wana uwezo mkubwa ndani yao lakini hawako tayari kuchukua hatua kuishi na kuachilia uwezo huo na matokeo yake uwezo huo unafia ndani yao na kuiacha dunia ikiwa na ombwe mahali ambapo uwezo huo ulipaswa kutumika.,

Tafiti za kisayansi katika eneo la uwezo wa binadamu zinaonesha kwamba 90% ya uwezo wa binadamu hufia ndani yao, ni 10% tu ya uwezo huo hutumiwa.

Kwa sababu hiyo kitabu hiki kinakupa mwongozo wa mambo muhimu unayopaswa kuyafanya ili uweze kuishi uwezo wako kwa ukamilifu wa viwango vya juu na siku ukiondoka hapa duniani uache dunia ikiyafurahia maisha yako hapa duniani.

Kupitia kitabu hiki utajifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na;-

- ✓ Aina 8 za uwezo wa kipekee, hii itakusaidia kujua aina yako ya uwezo na kuanza kuifanyia kazi.
- ✓ Jinsi ya kutambua eneo sahihi ya uwezo wako, hii itakusaidia kukaa eneo sahihi ili uwezo wako uonekane na kutoa matokeo
- ✓ Mambo muhimu ya kufanya pale ambapo uwezo wako unapita kwenye majaribu/changamoto, hii itakusaidia kutokata tamaa kwa sababu ya changamoto unazokutana nazo.

- ✓ Nguvu ya watu katika kukuza au kuua uwezo wako, hii itakusaidia katika kufanya uchaguzi wa watu wa kuwa nao katika safari ya kuishi uwezo wako
- ✓ Jinsi ya mtzamo wako unavyoweza kuathiri uwezo wako, hii itakusaidia kujenga mtazamo sahihi utakoa kusaidia kukuza uwezo wako.
- ✓ Namna 7 za kufikiri ili kukuza uwezo wako, hii itakusaidia kuwa makini na fikra zako ili usiue uwezo wako.

Pamoja na mambo mengine mengi mazuri. Ndani yako kuna uwezo mkubwa sana na ukuu unaishi ndani yako. Ishi uwezo wako.